SEHEMU YA 5
JINSI YA KUOMBEANA

LENGO: KUELEWANA KATIKA SALA TUNAPOOMBA NA KUJITAHIDI KUWALETA WAPOTEVU KWA YESU.

1. MBONA SISI WAKRISTO TWAHITAJIANA KATIKA SALA TUNAPOWAHUBIRIA WAPOTEVU KWA NIABA YA YESU?

A. Kwa kuwa uenezi wa injili waokoa roho kutoka utawala wa shetani (Wakolosai 1:13) shetani atajaribu kutuzuia kusali na kuwaleta wapotevu kwa Yesu kwa kututatiza sisi binafsi.
B. Wale watu waliomo katika nchi ambapo hawajawahi kusikia kuhusu Yesu, wamekuwa katika utawala wa shetani tangu kuangamia kwa shamba la Eden (Waroma 5:18 na Yohana 3:18) na hatawaachilia bila mapigano.
C. Twaweza kutarajia shetani kutuchunguza, kutujaribu, na kutufanya tusiwe na nguvu, kutushughulisha na mambo mengine, tusiwe na ari katika vita vya kuokoa roho (Luka 22:31-32)
D. Twahitaji silaha za kiroho kushinda vita hivi visivyo vya dunia hii, (2 Wakorinto 10:3-5)
E. Katika sala ya Bwana, Yesu alitufundisha tumwombe Bwana atuokoe kutoka kwa yule mwovu. (Matayo 6:13)
F. Neno la Mungu laiamuru kama sehemu ya silaha ambazo wakristo wahitaji katika vita vyetu vya kiroho dhidi ya shetani.
"Salini daima, mkiomba msaada wa Mungu. Salini kila wakati kwa nguvu ya roho. Kesheni bila kuchoka mkisali kwa ajili ya watu wa Mungu. (Wakristo) Waefeso 6:18

G. Ni sala zetu kwa Mungu, si kwa usaidizi wa kibinadamu, ambazo ndizo huleta ulinzi na matokeo. (Yakobo5:16)

II TUOMBEANENI KWA AJILI GANI?

A. Kwa ulinzi. (1 Watesalonike 3:1-3)
B. Kwa malaika watulinde. (Zaburi 91:11-12)
C. Kwamba sisi Wakristo tuwe na sifa na wale walioko nje ya kanisa. (1 Timoteo 3:7)
D. Kwamba tusiwe waoga katika kutii mwito wa Kristo kuwaokoa wapotevu. (2 Timoteo 1:7)
E. Kwamba hatutazuiwa na shetani katika kazi yake (1 Watesalonike 2:18)
F. Kumpinga shetani na majaribu yake yote. (Yakobo 4:7)
G. Kwamba tutakuwa wajasiri na kushirikiana katika injili. (Waefeso 6:19-20)
H. Tuwe macho wakati wote. (1 Petero 5:8-9, Wakorinto 10:12, Matayo 26:41).
I. Kushinda mashtaka ya shetani (Ufunuo 12:10-11)
J. Tuwe macho na kumpinga shetani anapokuja akinguruma kama simba. (1 Petero 5:8-9)
K. Tusianguke majaribioni. (Waebrania 2:18)
L. Kutumia mamlaka ya jina na damu ya Yesu. (Soma sehemu ya 4)

III TUTUMIE NJIA ZIPI KUOMBEANA?

A. Na kikundi chako cha watu watatu:
   1. Waombee wenzako wawili katika kikundi kila siku.
   2. Ukubali na uwasilishe kwa simu mahitaji unayotaka yaombewe na wenzako wawili wa kikundi.
   3. Hata hivyo msisahau kuwaombea wale ambao hawajaokoka mnapoombeana

B. Ombeni katika MAKUNDI YA SALA yaliyoko, au undeni mengine yoyote mapya mnayofikiri yahitajika kutosheleza matakwa yenu ya sala.
C. Jiungeni, na mwanzishe MPANGO WA SALA KWA SIMU katika kanisa shirika au jamii. (Tazama masharti)
    1. Wasalini kwa imani, wote wanaotaka waombewe wanapowaombea na kuwafikia wapotevu.
    2. Taja mahitaji yako maalum ili wengine waweze kukuombea.
D. Undeni mpango wa saa 24 wa kuombeana kwa simu kunapotokea haja maalum ya kuwaombea wapotovu.
    1. Chora mviringo mkubwa na kuugawa katika viwango vya muda wote wa saa 24.
    2. Kila mwombaji huchukua muda kulingana na vile anvyoahidi kuomba kila siku.
    3. Kila muombaji husali wakati sawa kila siku hadi mradi wa maombi kwa saa ukamilike.

IV WAEFESO 6:18 HUSEMA TUOMBEANEJE?

Isome ukiomba na kwa makini kwa majibu haya:

A. Hakikisha kwamba ni maombi halisi, wala siyo tu maongezi yanayo wahusu.
B. Salini kila wakati, ikiwa pamoja na makundi ya maombi na pia katika sala zako za faragha. (1 Watesalonike 5:17)
C. Rohoni, tukiongozwa na Roho Mtakatifu ndani yetu, kwa mapenzi ya Mungu, wala siyo yetu wenyewe. (Waroma 8:26-27)
D. Tuwe macho wakati wote. (Matayo 26:40-41, na 1 Petero 5:8)
E. "Kwa uvumilivu wote" - maana yake ni kushikilia kinidhamu, na sio tu kuomba kwa kugutukia bila mpango na utaratibu. (Luka 18:1)
F. Hoja za sala - maana yake ni kusalia maombi maalum kwa mahitaji maalum.

MAZOEZI

1. Amua pamoja na wenzako wawili wa kikundi chenu cha maombi wakati na jinsi mtakavyoombeana. (Si katika wakati wa maombi ya kikundi) kama kuwasiliana kwa simu.
2. Tayarisha, au jiunge na kundi la maombi kwa simu kanisani mwako au katika shirika lako, ili uwe ukiwaombea wengine kisha nao wakuombee.
3. Shiriki katika mpango wa maombi wa saa 24 kwa maombi maalum na shuguli za kueneza injili.
4. Anza kuomba mara moja katika makundi yako ya usaidizi.

SALA YAKO

1. "Baba, nayatoa mahitaji yangu kwako na kwa wale ambao wameahidi kuniombea."
2. "Baba, sasa nayaombea mahitaji ambayo washirika wangu wameniambia. (Taja mahitaji yenyewe)
3. "Nakuahidi, sio hao, Baba mpendwa kwamba nitawaombea kwa imani hawa ambao nimejitolea kuwaombea."

SHERIA KWA WANACHAMA WA USHIRIKA WA MAOMBI

1. MAOMBI YA SALA YANAYOPOKEWA
   A. Maombi ya kusaliwa yaweza kutoka mahali popote. (Wanachama wa ushirika wa maombi, wale wanaohitaji kuombewa, makasisi, halmashauri za kanisa, walimu na kadhalika.)

   B. Watakao kuombewa wampigie simu: (Nambari ya simu ya mwenyekiti)
   Ikiwa haijibiwi: (Nambari ya simu ya naibu wa mwenyekiti)
      1. Ikiwezekana simu za kuomba sala zipigwe kati ya saa moja na nusu asubuhi na saa tatu na nusu asubuhi.
         (a) Mwenyekiti kisha atawaarifu washirika wa ushirika wa asubuhi mara moja.
         (b) Ushirika wa jioni nao utatayarishwa jioni hiyo. Simu za dharura zaweza kupigwa wakati wo wote.
   C. Toa tu maelezo unayotaka yawasilishwe.

II MAAGIZO KWA WANACHAMA WA USHIRIKA WA MAOMBI WANAPOPOKEA SIMU.
   A. ANDIKA ombi la sala VILE unavyolipokea, neno kwa neno. (Tumia kitabu kinachotolewa kwa ombi na tarehe, na, jibu na tarehe)
      1. Toa tu maelezo uliyoyapokea kwa simu.
      2. Usiyapotoze maelezo hayo.
      3. Usitie dakizo kuhusu ombi la sala unalolipokea kwa simu.
   B. MPIGIE SIMU MARA MOJA MTU AFUATAYE KATIKA ORODHA YA WANACHAMA WA USHIRIKA WA MAOMBI.
      1. Ikiwa simu haijibiwi, uendelee kupiga simu ukifuata orodha hadi utakapojibiwa, na hivyo kuendeleza ushirika huo. (Waweza kuwapigia simu wale ambao hawakuwepo ulipopiga simu awali kuwaarifu, lakini hii si sharti. Amua kwa busara ya kikristo kuhusu jambo hili.)
   C. SALI MARA MOJA kuhusu maombi baada ya kupiga simu
      1. Usiiache simu yako hadi umeomba, ili usianze kufanya mambo mengine na hivyo kuiahirisha sala hiyo, au kuisahau kabisa.
      2. Omba mapenzi ya Mungu. (Usiombe majibu, sali maombi kwa Mungu.)
      3. Sali kwa bidii. "Sala ya mtu mwema ni nguvu ya kutenda mengi.' Yakobo 5:16

III WAWEZA KUWA CHOMBO KINACHOSUKUMA MKONO WA MUNGU. TUMIA BUSARA YA KIKRISTO KUWEKA MAOMBI HAYA SIRI.

IV MWARIFU MWENYEKITI, MAJIBU YANAPOPOKEWA. Haya pia yatajulishwa wanachama wa ushirika wa maombi ili kuwatia moyo.

Sahihi _____

Ukipata, wakati wowote kwamba sheria hizi ni ngumu kuzifuata, tafadhali mpigie simu mwenyekiti ili aliondoe jina lako kutoka ushirika huu wa maombi.

MAAGIZO KWA UJUMLA - Yasishirikishwe na sheria kwa wanachama wa ushirika wa maombi.

1. Ushirika wa sala wapasa uwe na wanachama 10. Madhumuni ya ushirika ni kuwawezesha watu wengi iwezekanavyo kuanza kusali mara moja. Gawanyeni katika makundi ya ushirika wa sala inavyowezekana.
2. Wape wanachama karatasi zilizochapishwa wazitumie kuweka rekodi za maombi ya sala na tarehe yanapopokewa majibu.
3. FANYENI MKUTANO WA MIPANGO ambapo KILA MWANACHAMA:-

(1) atatia sahihi sheria zilizoko hapo juu, na (2) hufanya sala fupi ya kujitolea KWA MUNGU, akimwahidi kwamba atakuwa akipiga simu na kusali mara tu ombi linapopokelewa.

4. Kutana mara kwa mara na wanachama wa ushirika wa sala, KUSALI PAMOJA na hivyo kuhifadhi hamu, na lengo la ushirika wazi. Maswali yanaweza kujibiwa, na matatizo kutatuliwa katika mikutano hii.